Hamanisha Kuu
(The Major Menaces)

Na

John Kombo

Hamanisha Kuu
(The Major Menaces)

Na

John Kombo

October 4, 2012

Hamanisha Kuu

Kwa muda wote toka nilipoanza kuhubiri na kumtumikia Bwana kumekuwa na swali ambalo nimeuliza: “Kama Mungu anahitaji watu wote wapewe nafasi ya kukubali mwaliko wake na amelipa gharaama kwa wote, na kama ametoa vyombo vya kufundishia kwa wote, kwa nini kuna wengi waliopotea leo.

Kikamilifu, jibu katika maswali yote hapo juu ipo katika sehemu mbili; hataivyo sababu ya kwanza ni zaidi ya uwezo wetu kubadilisha.

- Kwanza, wengi wanasikia kweli na kuikataa leo hata katika karne ya kwanza.
- Pili, wengi hawaja sikia kwa sababu watoto wa Mungu au watumishi wanashindwa kuwafikia.

Natarajia kuleta baadhi ya hamanika katika kutimiza kazi ya Bwana wetu. “*…chakula change ndicho hiki niyatende mapenzi yake aliyenipeleka nikamalize kazi yake. Hamsemi ninyi bado miezi mine, ndipo yaja mavuno? Tazama mimi nawaambieni inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno.*” (Yoh. 4:34-35).

“*Kawaambia mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache, basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake.*” (Luka 10:2).

- Ukosefu wa maono: kulikuwa ukubwa na ukuaji mkubwa wa kanisa na wahubiri kadha Antiokia. Roho Mtakatifu ulilipima kanisa hilo katika kufikiria kwamba kanisa hilo lilikuwa linakuwa nyumbani kulikuwa na hitaji la kutuma watenda kazi katika mavuno ulimwenguni (Mdo. 13:1-3). Mara zote tunafikiria kwamba kwa vile kuna kazi njema nyumbani; haijalishi kwamba watu wa sehemu zingine hawana nafasi ya kusikia hata somo moja kuhusu Yesu.
- Injili mara nyingi huamanishwa kwa sababu ya msisitizo wa uongozi mbaya katika kazi zetu. Wakati wamiosionari wanapotumwa msisitizo haupaswi tu kuanzishwa kwa makusanyiko, ili kuifanya yenyewe ijitegemee kwamba sio sahihi. Tuweke macho yetu katika dunia yote iliyopotea. Mikakati ya majengo na watu ni njia pekee ya kuwafikia waliopotea, siyo mwisho wake.
- Hamanisho la tatu. Kwa wengi wetu hakuna kitu cha kuhogofywa kuliko yenyewe. (Mat. 4:1; 1 Fal. 19:10). Katika wakati wa kwanza wa kusikika kwa Danieli Rumi kila mmoja alimuacha. Hataivyo,

katika nyakati hizo za upweke, Bwana alisimama pamoja naye na kumtia nguvu kwamba Wayunani wote waweze kusikia injili ya Yesu Kristo. Hivyo, Wakristo wote wanapaswa kutambua kwamba Bwana yuko pamoja nao kila wakati wanaposafiri katika dunia yote kutangaza habari njema. (Mdo. 17:6; 1 Thes. 3:1-3).

- Kutovutiwa. Baadhi ya watu na makanisa wanakuta kwamba ulimwengu wenye dhambi hawamgeukii Mungu kirahisi; hivyo wanaacha kazi kwa sababu ya kukata tamaa. Tunashindwa kuwafikia watu mara nyingi kwa sababu tunahubiri mafundisho ya kweli lakini tunakataa ukweli mwingine ambayo hutimiza mahitaji ya ndani. Mahitaji yote ya watu fulani, Kristo anayatimiza.

- Ubinafsi ni hamaniko ambayo mara zote huongoza katika mgawanyiko katika kazi. Wafanya kazi wengine wanajaribu kuunda wazo la kujenga ufalme binafsi. Wanajikinga na chuki tofauti. Wakati mwingine wanaogopa kuwasiliana na waongofu kwa wahubiri fulani ambao wakristo wachanga wanaweza kuvutiwa nao sana kuliko wao. Ubinafsi kwa njia yoyote itgashinda; mfano kwa Diotrefe ambaye alitamani kutokuwa na hamaniko ya kanisa na alikuwa na wivu dhidi ya Yohana (3 Yohana).

- Kumfanyia kazi mkuu asiye sahihi pia ni hamaniko nyingine. Wengine wanahisi kwamba wanaifanyia kanisa kazi nyumbani, kwa sababu wanalipwa mishahara na makanisa hayo. Wanamfanyia Bwana kazi. Mara zote tunapaswa kukumbuka kwamba tunamfanyia Mungu kazi ambaye ndiye mwajiri wetu (Mdo. 4:19-20).

- Kujiingiza katika mambo ya kimwili ni kutingwa na ni hamaniko kwa wainjilist wa dunia. Takwa la kuwa tajiri ni hatari (1 Tim. 6:5). Paulo anasema ni mtego, ambao mwanadamu anajiingiza mwishoni, na mwanadamu anachomwa na huzuni kama mshale kuonyesha uhatari wake. Kupenda utajiri wa kimwili husababisha waumini kukadiria kwa njia nyingi. Kwa mfano, wengi wanabisha kwamba wanaweza kufanya zaidi mema wakitengeza fedha na kutoa fedha kuliko kufundisha.

- Ukosefu wa imani ni hamanisho kubwa katika uinjilist. Tunapokuwa na imani tunakuwa na tumaini. Imani ni kuukubali neno la Mungu kwa wakati aliousema. Tunaimani kwa Mungu kwa sababu amesema dhambi inauwa na kwamba wote wamekufa (Rum. 6:23, Rum. 5:12). Hatupaswi kujisemea

wenyewe na kufikiria kwamba jirani katika mlango unaofuata na yule mgeni wa mbali wataokolewa pasipo Yesu.

- Hamanisho la mwisho labda ni kubwa kuliko vyote. Hii ni rahisi tu kuto kwenda. Mungu hatuambii kujaribu kuifanya kazi hii eti kwa sababu tunajihisi kwamba tunaweza kuifanya. Anatutaka sote kuifanya kazi yake kwa sababu inaitajika ifanyike, alafu atatusaidia. Tunapaswa kukumbuka kwamba tukitumia uwezo wetu, Mungu atatutumia.

Kuhitimisha, sote tukumbuke, siku ya hukumu. Mwana kondoo wa Mungu akitua mawinguni mbele za watu wote wa karne zote, rangi, kabila, unakotoka, n.k. vitabu vitafunuliwa. Kila maisha ya kila mtu itachunguzwa katika maisha ya hadithi ya Mungu (Ufu. 20:12, 2 Kor. 5:10).

Kuna wale wanaomkataa Yesu waziwazi. Wanakataa neema iliyotolewa ya Baba wa upendo.

Mamilioni ambao hawakusikia wanatazama deni katika ufalme wa Bwana. Wanajitahidi kuelewa tukio hili – ukumu ya Mungu – milele. Wengine wanajiangalia wenyewe waumini na kusimama wakisubiri huruma hii ya milele. Lakini Yesu anawaambia "*Ondokeni kwangu sikuwajua ninyi.*" (Mat. 7:21).

Mungu Baba yetu mpendwa, tusaidie na utupe hekima zaidi, nguvu na zaidi ya yote upendo wa neno lako.

Wenu katika Upendo wa Kristo

John Kombo Nandwa

Kanisa la Kristo Barut

Nakuru, Kenya